

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA NNE

06 APRILI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA NNE – TAREHE 06 APRILI, 2018

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**24. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON
MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini ujenzi unaoendelea katika Vituo vya Afya Ikuti Wilayani Rungwe na Ipinda Wilayani Kyela utakamilika ili kuwawezesha Wananchi wa maeneo hayo kupata huduma kwa wakati.

**25. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia vikundi vya Wanawake waliopo katika Mkoa wa Rukwa katika suala la mikopo na kuwapatia elimu ya ujasiriamali.

**26. MHESHIMIWA OMAR ABDALLAH KIGODA
(HANDENI):-**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la Wagonjwa (*ambulance*) katika Hospitali ya Handeni hasa ikizingatiwa kuwa Hospitali hiyo inahudumia Wagonjwa wengi kutoka takribani Majimbo manne.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

27. MHESHIMIWA AMINA NASSORO MAKILAGI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Zipo Sheria nyingi ambazo zimepitwa na wakati na Sheria nyingine ni kikwazo katika kufanikisha shughuli muhimu za Taifa letu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzitambua Sheria zote zilizopitwa na wakati na zile zinazochelewesha ukuaji wa uchumi.

28. MHESHIMIWA ISSA ALI MANGUNGU (MBAGALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

- (a) Je, Mabaraza ya Wazee katika Mahakama za Mwanzo yapo kwa mujibu wa Sheria;
- (b) Mahakama ya Mwanzo Kizuiani hulipa posho za Wazee wa Baraza kiasi cha Tshs.5000/= kila wanapomaliza Shauri; Je, kwa nini sasa yapata miezi 9 Wazee katika Mahakama ya Mwanzo Kizuiani hawajalipwa posho zao.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

29. MHESHIMIWA MGENI JADI KADIKA (VITI MAALUM):-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Imekuwa ni mazoea sasa Vijana wetu wengi hasa wa kike wanapokwenda kufanya kazi za ndani katika nchi za Uarabuni kama vile Oman, Dubai na Saudi Arabia kunyanyaswa na kuteswa na hata wakati mwingine wanauawa.

Je, inapotokea kadhia hiyo kwa nini Balozi wetu anaewakilisha nchi yetu hatoi taarifa mapema na inachukua muda mrefu kujulikana.

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

30. MHESHIMIWA JORAM ISMAEL HONGOLI (LUPEMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Katika Jimbo la Lupembe Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Tarafa ya Lupembe hususan Kijiji cha Madeke kinazalisha matunda aina ya Nanasi, Parachichi na matunda mengine lakini hakuna soko la matunda hayo na

hii ni kutokana na kutokuwa na Kiwanda kikubwa cha matunda:-

(a) Je, Serikali inasaidiaje upatikanaji wa masoko ya mazao hayo;

(b) Je, ni lini Serikali italeta Kiwanda katika eneo hilo.

31. MHESHIMIWA DAVID ERNEST SILINDE (MOMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Katika kutekeleza azma ya Tanzania ya viwanda:-

Je, Halmashauri ya Momba inatarajiwa lini kujengewa Kiwanda na ni cha aina gani.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

32. MHESHIMIWA JUSTIN JOSEPH MONKO (SINGIDA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya Singida - Ilongero-Mintiko hadi Hydrom inayounganisha Mikoa ya Singida na Manyara ni kiungo muhimu katika kusafirisha mazao ya Wakulima na bidhaa

za Wafanyabiashara na inapita katika Hospitali ya Rufaa ya Hydrom ambayo Wananchi hufuata huduma kwa kukosa Hospitali ya Serikali katika Halmashauri:-

Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami ili kunusuru maisha ya Wananchi wa Singida Kaskazini.

33. MHESHIMIWA DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (SONGEA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Serikali ya Awamu ya Tano imeusaidia sana Mji wa Songea kwa kuleta ndege za Bombadier ambazo zinatoa huduma zake katika Uwanja wa Ndege wa Songea:-


- (a) Je, kwa nini uwanja huo hauongezwi urefu na kufanyiwa ukarabati ili kutoa huduma zaidi na kuruhusu ndege ziweze kutua kwa saa 24;
- (b) Je, kwa nini Serikali haiweki mashine za ukaguzi wa abiria (*scanning machine*) ili kuondoa adha kwa abiria kukaguliwa mizigo yao kwa kupekuliwa ambapo inadhalilisha na kupoteza muda.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

(Majadiliano yanaendelea)



DODOMA
06 APRILI, 2018

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE